# " ULEMAVU BARANI AFRIKA"
# EPISODE 9: "Weka kitu cha kukumbukwa"

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo**

**List of characters / Episode 9:**

**MSIMULIZI**

**<u>SCENE ONE: MORNING AT OLUANDA'S HOME</u>**

- Oluanda (mume, 18)
- Tofa (mke, 40)

**<u>SCENE TWO: IN THE MALI'S LIVING ROOM</u>**

- Kangwa (Mke, 18)
- Mr. Mali (mume, 50)
- Mrs. Mali (mke, 45)

**<u>SCENE THREE : KANGWA IN THE HEADTEACHER'S OFFICE</u>**

- Kangwa (Mke, 18)
- Mrs. Nina (mke, 45)

**<u>SCENE FOUR: AT MAGANYE MARKET- PLACE</u>**

- Oluanda (mume 18)
- Gidi (mume, 38)
- Inspekta Joe (mume, 30)
- Wema (mke, 40)
- Crowd (wake na waume umri mchanganyiko)

**SCENE FIVE: CHITOTO DRUNK ON WAY HOME**

- Chitoto (mume, 19)
- BW. Mali (mume, 50)
- BI. Mali (mke, 45)

**UTANGULIZO:**

Nakusalimu na kukukaribisha katika kipindi cha Noa bongo,jenga maisha yako. Hiki ni kipindi cha tisa tukiangazia “ **Walemavu barani Afrika** ”. Tulipoachana,Tuliihitimisha hadithi yetu wakati Bw. Mali akimuhakikishia Oluanda kwamba atawashawishi wafanyi biashara na hata waandishi wa habari kutoka ng’ambo kuja kuchukua habari za maandamano na kujiunga nao. Fauka ya hayo, Chitoto amegunduwa kuwa Kangwa na Oluanda ni zaidi ya kuwa walisoma pamoja,Kangwa ameanza kumleta karibu Oluanda. Jambo hilo lilimfanya Chitoto amchukie zaidi Oluanda. Na je kuhusu Bi.Mali? akisikia habari hizi atasemaje? Maandamano hayo yatafaulu? Tulia usikilize kipindi hiki, kwa jina “**Kuweka historia**”. Tunalifunguwa jamvi asubui mbichi nyumbani kwa kina Oluanda.

**SCENE ONE : MORNING AT OLUANDA’S HOME**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | **SFX:** | **MORNING AMBIENCE FOLLOWED BY WASHING FACE WITH WATER FROM BASIN** |
| 2. | **TOFA:** | Oluanda, kijana wangu una nguvu za ndovu kumi, na moyo wa simba. Ni ngumu kufikiria kuwa unajifanyia kila kitu peke yako na ilihali ni miezi michache tu ulikuwa umekufa moyo, bila tumaini la kutimiza ndoto zako. |

3. **OLUANDA:** Najua mama, lakini nisingeliweza peke yangu bila wewe. Kuhusu ndoto zangu.. nataka kukuambia kuwa ninapanga kumuoa Kangwa.

4. **TOFA:** **(Overjoyed and almost in tears)** Mungu wangu…! Hizi ni…

5. **OLUANDA:** Usilie mama, na sio hilo tu. Iwapo tutafaulu na haya maandamano au la, nitarudi shule. Nataka kuweka historia Maganye kuwa muhandisi wa kwanza kutembea na magongo.

6. **TOFA:** **(Happy tears)** Nimefurahi sana mwanangu, kama mamako. Sasa umeshazungumza na Kangwa kuhusu hayo? Kwamba unataka kumuoa?

7. **OLUANDA:** **(Chuckles)** Ndio. Jana alikuja kuniona na babake, kisha babake alipoondoka, nikamueleza lakini tukakubaliana kuwa kwanza tumalize masomo kisha ndio tufunge ndoa,

8. **TOFA:** Siamini kama ni ukweli! Nawatakia kila la heri nyote. Na amewaeleza wazazi wake kuhusu hayo?

9. **OLUANDA:** Alinihakikishia atawaeleza asubui kabla ya kwenda shule. Bila shaka saa hizi anawaeleza….

10. **NARRATOR:** Oluanda hakukosea katu, Kangwa alikuwa ameshawaeleza wazazi wake kuwa angelitaka kufunga ndoa na Oluanda, tofauti ni kuwa, habari hizi zilipokelewa tofauti na jinsi mamake Oluanda alivyozipokea. Usibanduke karibu na redio ujue kulijiri nini.

**SCENE TWO: IN THE MALI'S LIVING ROOM**

| | | |
|---|---|---|
| 11. | **SFX:** | **ROOM AMBIENCE** |
| 12. | **BI. MALI:** | **(Screams out)** Kangwa! Unamaanisha nini? Wataka kunipa maradhi ya moyo?Unataka kuolewa na kiwete anayeshona viatu kupata riziki? |
| 13. | **BW.MALI:** | **(Calmly)** Mke wangu, huko ni kukufuru sasa. Nimekutana na huyo kijana na sikuona ubaya wake. |
| 14. | **BI.MALI:** | **(Maliciously)** Nyinyi wawili mumepanga kuniangamiza, sindio?. Basi hamutaniua ng'oo! |
| 15. | **KANGWA:** | Mama, najua haumpendi Oluanda lakini ni yeye nimemchaguwa . Tafadhali elewe hivyo na umkubali. Nikiwa na yeye huwa siuoni ulemavu wake… huona nguvu na ukamilifu wake… |

16. **BI.MALI:** **(Loudly)** Utakosaje kumuona mkamilifu na yeye ashakuroga mwanangu Kangwa! Hamulioni hilo? Yule anaukodolea macho huu utajiri wetu tu!

17. **KANGWA:** **(Angry)** Siwezi kusimama hapa na kusikiza zaidi. Mama sio kila mtu mwenye haja ya mali na pesa. Wengine wanataka kunufaisha maisha ya wenzao, basi .Naenda zangu shule. Kwaheri baba. Tuonane kesho kwenye maandamano.

18. **BW.MALI:** Sawa. Tuonane huko na ni kama nilivyopanga itakuwa sherehe kubwa.

19. **KANGWA:** Shukran. Natamani mama angelikuwa na mtazamo kama wako….

20. **MSIMULIZI:** Kangwa alifulizia shuleni na moyo mzito, lakini kabla aingie darasani kwake, aliiitwa na mwalimu mkuu. Alimwendea Bi.Nina na shauku na dukuduku moyoni.

**SCENE THREE: KANGWA IN THE HEADTEACHER'S OFFICE**

21. **SFX: ROOM AMBIENCE; COMPUTER**

22. **BI.NINA:** Nimepokea simu nyingi kutoka kwa wanahabari na wanasiasa wakitaka kujua zaidi kuhusu Oluanda. Inaonekana maandamano haya yanasubiriwa na wengi na yameibua

matamanio ya wengi. **(Happily)** Nataka mujue kesho nitajiunga nanyi mimi na familia yangu. Ninajuta kumfukuza shule Oluanda. Labda hili litampa ufunuo zaidi.

23. **KANGWA:** **( Excited)** Asante mwalimu. Nina hakika Oluanda na walemavu wote Maganye watashukuru.

24. **BI.NINA:** Ni hayo tu. Unaweza kurudi darasani.

25. **SFX :** **DOOR CLOSED**

**26. MSIMULIZI:** Kangwa hakuamini masikio yake. Alitoka afisini mwa mwalimu mkuu na tabasamu kubwa akirudi darasani mwake. Katika soko la Maganye, walemavu wengine wakiongozwa na Wema, mlemavu na mzazi wa watoto wawili, bado walikua wakimsumbuwa Gidi kuhusu mkutano wa maandamano uliopangiwa kufanyika siku iliyofuatia.

**<u>SCENE FOUR: AT MAGANYE MARKET- PLACE</u>**

27. **SFX:** **MARKET AMBIENCE**

28. **GIDI:** **(Stress)** Sikizeni! Nimewaambia sijui! Hili lilikuwa wazo la Oluanda hata hivyo. Muulizeni yeye kama maandamano yako au la!

29. **SFX:** **MURMURS AND SHOUTS FROM CROWD**

30. **WEMA:** Nilijuwa! Hii ilikuwa njama tu ya

| | | |
|---|---|---|
| | | kutufedhehesha na kututumia. Wewe na Oluanda sasa mumetajirika na kujulikana na kusahau haki zetu na maandamano. |
| 31. | **SFX:** | **MORE SHOUTS AND LOUD PROTESTS FROM ANGRY CROWD** |
| 32. | **GIDI:** | Wema una wazimu? Unafikiri ningeliketi hapa nikiombaomba kama ningelikua na pesa usemavyo ? |
| 33. | **WEMA:** | **(Angry tone)** Ndio. Kutudanganya! Tutajuaje, labda una pesa za kutosha lakini umekaa hapa kutukejeli sote tukiwa tumebeba mabango yetu na matawi tayari kwa maandamano. Umehongwa na wanasiasa! **(With a realization)** Oluanda yule yuaja… na askari? ameshikwa!...mmh mimi simo!!!!. |
| 34. | **SFX:** | **CROWD STARTS PANICKING** |
| 35. | **GIDI:** | **(Shouts out)** Wema ngoja, subirini jamaa, tulieni! Yule ni Inspekta Joe kutoka kituo cha polisi cha Maganye .Mbona munamuogopa? Hakuna makosa muliofanya. Tuna haki ya kujumuika pamoja hata kama sisi ni walemavu. |
| 36. | **OLUANDA:** | **(Happy tone)** Ndugu zangu,nina habari njema kwenu! |

37. **INSP.JOE:** Kibali chenu cha maandamano yenu kesho hiki hapa. Hata hivyo tutakuwa hapo kuhakikisha sheria, amani na utulivu unadumishwa. Inaonekana kilio chenu kimefikia watu wakubwa serikalini. Kila la heri hapo kesho.

38. **SFX:** **HUGE WILD APPLAUSE FROM CROWD**

39. **MSIMULIZI:** Kwa muda, soko la Maganye lilijawa na sauti za furaha, shangwe na vigelegele za walemavu walioungana, kuwa pamoja na tayari kuyakabili matatizo yalio mbele yao. Magongo yaliinuliwa juu kwa furaha na hata pia fimbo za vipofu , vigari vilizungushwa mduara na kulifanya soko kutouzika kwa muda. Oluanda aliwasalimu na kuwakumbatia wote, kisha akarudi nyumbani akiwa na furaha pomoni. Kwengineko, Chitoto ametoka shule kwenda nyumbani lakini njiani……..

**<u>SCENE FIVE: CHITOTO DRUNK ON WAY HOME</u>**

40. **SFX:** **SEVERAL GULPS OF A DRINK FOLLOWED BY A BURP**

41. **CHITOTO:** **(Cursing with drunken tone )** Oluanda! Oluanda… vile nachukia… aah hata hivyo sina haja na yule sura mbaya Kangwa. Bora nipate chupa nyengine. Ala, kilabu kile.. acha nivuke Barabara..

42. **SFX:** **EMERGENCY BREAK FROM CAR**

| | | |
|---|---|---|
| 43. | **BI. MALI:** | **(Screams out)** Wuuuuuuiiiiiii! Mali, Umegonga mtu! Umeua!!!! |
| 44. | **BW. MALI:** | **(In a panic)** Sikumuona! Naapa sikumuona sijui ametokeza vipi barabarani.. |
| 45. | **BI. MALI:** | Basi fanya kitu..usizubae tu hapo fwee umeshika usukani. |
| 46. | **BW. MALI:** | Niletee kisanduku changu cha huduma ya kwanza kutoka kwa buti la gari.. haraka… |
| 47. | **SFX:** | **CAR DOORS OPENED SIMULTANEOUSLY** |
| 48. | **BW. MALI:** | Kijana?… umeumia? Amka..? |
| 49. | **BI. MALI:** | Ni mzima?...jamani…ananuka pombe. |
| 50. | **BW. MALI:** | Ndio, ni mzima, ameshituka tu, ni bahati nimefunga breki kwa wakati, bahati pia amepata majeraha kidogo mguuni, dawa za maumivu zitamfaa kabla afike hospitali kuangaliwa zaidi… |
| 51. | **BI. MALI:** | Lakini huyu si ni mdogo sana kuanza ulevi? Angelikuwa amekufa leo! |
| **52.** | **BW. MALI:** | Ndio, lakini tusijadiliane hayo kwa sasa… nipe dawa kwanza.. |
| 53. | **SFX:** | **PLASTIC FIRST-AID BOX OPENED** |

| | | |
|---|---|---|
| **54.** | **BW. MALI:** | Hebu nisaidie kuvaa glavu. |
| 55. | **SFX:** | **LATEX GLOVES STRETCHED AND WORN** |
| 56. | **BW. MALI:** | Sasa rudi ukaangalie gari…. Sitaki tena ajali nyengine… |
| **57.** | **BI. MALI:** | Lakini mume wangu ni sisi tu wenye gari hapa umesahau? |
| **58.** | **BW. MALI:** | **(Commanding)** Nimesema rudi kwenye gari! Umesikia? |
| 59. | **BI. MALI:** | Haya. Ni sawa. |
| 60. | **SFX:** | **LIQUID SHOOK IN BOTTLE** |
| **61.** | **CHITOTO:** | **(Cries from sting of antiseptic )** Arrrrrgh!...Nini …niko wapi? Kumetokea nini? |
| **62.** | **BW.MALI:** | Kijana afadhali umeamka. Uko Maganye, katikati ya barabara na una bahati sana, karibu nikugonge kwa gari yangu. Unahisi maumivu mahali popote? Itakubidi twende hospitali… |
| 63. | **CHITOTO:** | Wewe… wewe ni nani? |
| **64.** | **BW.MALI:** | Mimi, sawa.. nitakueleza baadae .. unahisi maumivu pahala popote? |

| | | |
|---|---|---|
| 65. | **CHITOTO:** | Nahisi … kisunzi lakini niko sawa. Mbona niko hapa? |
| 66. | **BW.MALI:** | Hebu njoo ;twende hospitali.nitakujibu maswali yako yote. **(Calls out)** Mama Kangwa! ingia garini. |
| 67. | **SFX:** | **CAR DOORS CLOSED, ENGINE STARTS AND DRIVES AWAY.** |

**<u>HITIMISHO:</u>**

Ilivyo Bw na Bi. Mali wakimpeleka Chitoto hospitali,tunatamatisha kipindi chetu cha tisa cha **" Walemavu barani Afrika" .** Je, Chitoto kweli hana neno kama anavyofikiri Bw.Mali? ama kuna la ziada? ni kina nani watakaokuja maandamanoni na matokeo yake ni yapi? Kwa haya na zaidi usikose kipindi chetu cha kumi na cha mwisho. Kusikiliza tena kipindi hiki au chengine tembelea tovuti zetu www.dw-world.de/lbe Usisahau kuwasiliana nasi wakati wowote. Kwa sasa twakutakia kila la heri.